

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



MKUTANO WA KUMI NA NNE

YATOKANAYO NA KIKAO CHA TATU

31 JANUARI, 2019

MKUTANO WA KUMI NA NNE

KIKAO CHA TATU – TAREHE 31 JANUARI, 2019

I. DUA:

Saa 3:00 asubuhi Mhe. Job Y. Ndugai (Spika) alisoma Dua na kuongoza Kikao cha Bunge.

IDADI YA WABUNGE WALIOHUDHURIA:

MAKATIBU MEZANI:

1. Ndg. Ramadhan Issa
2. Ndg. Zainab Issa
3. Ndg. Bakari Kishoma

II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

WAZIRI WA MAJI:

Aliweka Mezani Maelezo ya Waziri wa Maji kuhusu Muswada wa Sheria ya Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira wa Mwaka 2018 [*The Water Supply and Sanitation Bill, 2018*].

MWENYEKITI WA KAMATI YA KILIMO, MIFUGO NA MAJI:

Aliweka Mezani Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Kilimo, Mifugo na Maji kuhusu Muswada wa Sheria ya Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira wa Mwaka 2018 [*The Water Supply and Sanitation Bill, 2018*].

MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI KUHUSU WIZARA YA MAJI:

Aliweka Mezani Maoni ya Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani juu ya Wizara ya Maji kuhusu Muswada wa Sheria ya Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira wa Mwaka 2018 [*The Water Supply and Sanitation Bill, 2018*].

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:

Aliweka Mezani Maelezo ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria mbalimbali (Na. 4) wa Mwaka 2018 [*The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No. 4) Bill, 2018*].

MWENYEKITI WA KAMATI YA KATIBA NA SHERIA:

Aliweka Mezani Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Katiba na Sheria kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria mbalimbali (Na. 4) wa Mwaka 2018 [*The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No. 4) Bill, 2018*].

MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI KUHUSU WIZARA YA KATIBA NA SHERIA:

Aliweka Mezani Maoni ya Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani juu ya Wizara ya Katiba na Sheria kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria mbalimbali (Na. 4) wa Mwaka 2018 [*The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No. 4) Bill, 2018*].

III. MASWALI:

OFISI YA WAZIRI MKUU:

Swali Na. 26: Mhe. Cecilia Daniel Paresso

Nyongeza: Mhe. Cecilia Daniel Paresso

OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

Swali Na. 27: Mhe. Daniel Edward Mtuka

Nyongeza: Mhe. Daniel Edward Mtuka
Mhe. Justine Joseph Monko

WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO:

Swali Na. 28: Mhe. Catherine Valentine Magige

Nyongeza: Mhe. Catherine Valentine Magige
Mhe. Vedastus Mathayo Manyinyi
Mhe. Susan Limbweni Kiwanga

WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:

Swali Na. 29: Mhe. Rashid Abdallah Shangazi

Nyongeza: Mhe. Rashid Abdallah Shangazi
Mhe. Dkt. Steven Lemomo Kiruswa

**WIZARA YA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA
MASHARIKI:**

Swali Na. 30: Mhe. Othman Omar Haji

Nyongeza: Mhe. Othman Omar Haji

WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA:

Swali na. 31: Mhe. Oscar Rwegasira Mukasa

Nyongeza: Mhe. Oscar Rwegasira Mukasa

WIZARA YA KATIBA NA SHERIA:

Swali Na. 32: Mhe. Moshi Selemani Kakoso

Nyongeza: Mhe. Moshi Selemani Kakoso
Mhe. James Francis Mbatia

WIZARA YA MAJI NA UMWAGILIAJI:

Swali Na. 33: Mhe. Esther Lukago Midimu

Nyongeza: Mhe. Esther Lukago Midimu
Mhe. Eng. Christopher Kajoro Chiza
Mhe. Devotha Mathew Minja
Mhe. Mussa Bakari Mbarouk

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:

Swali Na. 34: Mhe. Zainab Athuman Katimba

Nyongeza: Mhe. Zainab Athuman Katimba
Mhe. Najma Murtaza Giga
Mhe. Goodluck Asaph Mlinga
Mhe. Dkt. Immaculate Sware Semesi
Mhe. Jacqueline Ngonyani Msongozi

WIZARA YA KILIMO:

Swali na. 35: Mhe. Joseph Michael Mkundi

Nyongeza: Mhe. Joseph Michael Mkundi

Swali Na. 36: Mhe. Joel Mwaka Makanyaga

Nyongeza: Mhe. Joel Mwaka Makanyaga
Mhe. Antony Calist Komu

IV. MATANGAZO:

WAGENI

Wageni mbalimbali waliokaa kwenye *galleries* za Ukumbi wa Bunge walitambulishwa na Mhe. Spika.

V. TAARIFA YA SPIKA:

Mhe. Spika alitoa taarifa ya ufafanuzi kuhusu taarifa nyingi anazotoa
Mhe. Zitto Zuberi Kabwe kwenye vyombo vya habari na mitandao ya kijamii ambazo zinaupotosha umma kwamba:-

- (a) Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kuhusu matumizi ya 1.5 trilion;
- (b) Barua aliyomwandikia Katibu Mkuu CPA;
- (c) Ukaguzi Maalum uliofanywa na CAG;

Mhe. Spika alieleza masikitiko yake juu ya upotoshwaji wa makusudi unaofanywa na Mhe. Zitto na kuwaomba Wabunge wajikite kwenye ushindani wenye tija na si kuendesha siasa za uongo na uzushi.

Pia, aligusia suala la Mhe. Tundu Lissu kuendelea kueleza vyombo vya Habari na Umma kuwa Spika na Bunge halijawahi kumjali kifedha toka alivyoanza matibabu jambo ambalo si kweli kwa kuwa mpaka sasa ameshahudumiwa kiasi kisichopungua shilingi milioni 250 na kwamba kuanzia sasa Ofisi ya Spika itaanza kujibu Hoja zake.

VI. MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI:

*(Kusomwa Mara ya Pili, Kamati ya Bunge Zima na
Kusomwa Mara ya Tatu)*

- (a) Mhe. Makame Mbarawa, Waziri wa Maji aliwasilisha maelezo kuhusu Muswada wa Sheria ya Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira wa Mwaka 2018 *[The Water Supply and Sanitation Bill, 2018]*;
- (b) Mwenyekiti wa Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji Mhe. Mahmoud Hassan Mgimwa aliwasilisha maelezo kuhusu Muswada wa Sheria ya Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira wa Mwaka 2018 *[The Water Supply and Sanitation Bill, 2018]*;
- (c) Msemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kwa Wizara ya Maji, Mhe. Hamidu Hassan Bobali aliwasilisha maelezo ya Kambi kuhusu Muswada wa Sheria ya Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira wa Mwaka 2018 *[The Water Supply and Sanitation Bill, 2018]*;

2. Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria mbalimbali (Na. 4) wa Mwaka 2018 [*The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No. 4) Bill, 2018*].
 - (a) Mwanasheria Mkuu wa Serikali aliwasilisha Maelezo kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria mbalimbali (Na. 4) wa Mwaka 2018 [*The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No. 4) Bill, 2018*];
 - (b) Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba na Sheria Mhe. Najma Murtaza Giga aliwasilisha Maoni na ushauri wa Kamati kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria mbalimbali (Na. 4) wa Mwaka 2018 [*The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No.4) Bill, 2018*];
 - (c) Mhe. Latifah Chande aliwasilisha Maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria mbalimbali (Na. 4) wa Mwaka 2018 [*The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No.4) Bill, 2018*].

Uchangiaji wa jumla ulianza na Wabunge wafuatao walipata nafasi ya kuchagua miswada iliyowasilishwa:-

- | | | |
|--|---|-----|
| 1. Mhe. Eng. Edwin Amandus Ngonyani | - | CCM |
| 2. Mhe. Justine Joseph Monko | - | CCM |
| 3. Mhe. Khadija Hassan Aboud | - | CCM |
| 4. Mhe. Edward Franz Mwalongo | - | CCM |
| 5. Mhe. Zitto Zuberi Ruyagwa | - | ACT |
| 6. Mhe. Dkt. Christine Gabriel Ishengoma | - | CCM |
| 7. Mhe. Mhe. Dkt. Steven Lemomo Kiruswa | - | CCM |
| 8. Mhe. Dkt. Raphael Masunga Chegeni | - | CCM |

KUSITISHA BUNGE:

Saa 7:00 mchana, Mwenyekiti wa Bunge Mhe. Andrew John Chenge alisitisha Shughuli za Bunge hadi saa 10:00 Alasiri.

BUNGE KUREJEA:

Saa 10:00 Alasiri Bunge lilirejea likiongozwa na Mwenyekiti wa Bunge Mhe. Andrew John Chenge.

Uchangiaji wa jumla uliendelea na Wabunge wafuatao walipata nafasi ya kuchagua miswada iliyowasilishwa:-

9. Mhe. Jitu Vrajlal Soni	-	CCM
10. Mhe. Antony Calist Komu	-	CHADEMA
11. Mhe. Hamidu Hassan Bobali	-	CUF
12. Mhe. Margareth Simwanza Sitta	-	CCM
13. Mhe. Najma Murtaza Giga	-	CCM
14. Mhe. Agnes Mathew Marwa	-	CCM
15. Mhe. Mussa Bakari Mbarouk	-	CUF
16. Mhe. Lucy Simon Magereli	-	CHADEMA
17. Mhe. James Francis Mbatia	-	NCCR

KUHITIMISHA HOJA:

1. Mwanasheria Mkuu wa Serikali alihitimisha Hoja yake kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 4) wa Mwaka 2018 [*The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No. 4) Bill, 2018*].
2. Waziri na Naibu Waziri wa Maji walihitimisha Hoja zao kuhusu Muswada wa Sheria ya Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira wa Mwaka 2018 [*The Water Supply and Sanitation Bill, 2018*].

KAMATI YA BUNGE ZIMA:

1. Kamati ya Bunge Zima ilikaa na kupitisha Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria mbalimbali (Na. 4) wa Mwaka 2018 [*The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No. 4) Bill, 2018*] Ibara kwa Ibara. Bunge lirejea na Mtoa Hoja Mwanasheria Mkuu wa Serikali alitoa Taarifa ya Kamati ya Bunge Zima na kisha alitoa hoja iliyoungwa mkono. Bunge lilirejea na Hoja iliamuriwa na kuafikiwa na Muswada ulisomwa kwa Mara ya Tatu.

2. Bunge lilikaa kama Kamati ya Bunge Zima kuupitisha Muswada wa Sheria ya Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira wa Mwaka 2018 [*The Water Supply and Sanitation Bill, 2018*], Ibara kwa Ibara pamoja na marekebisho yake. Bunge kurejea na Mtoa Hoja Waziri wa Maji alitoa Taarifa ya Kamati ya Bunge Zima na Bunge lilihojiwa ambapo hoja iliamuriwa na kuafikiwa na Muswada kusomwa Mara ya Tatu.

KUAHIRISHA BUNGE:

Saa 1:15 usiku Mwenyekiti wa Bunge Mhe. Andrew John Chenge aliahirisha Bunge hadi siku ya Ijumaa tarehe 1 Februari, 2019 saa 3:00 asubuhi.